**MWONGOZO KIS PP2 BUNAMFAN CLUSTER EXAMS 2022**

**UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

(a) Uvutaji sigara/tumbaku.
Madhara ya uvutaji sigara/tumbaku **(alama 1x2=2)**

(b) (i) Husababisha saratani
(ii) Husababisha shida za macho na masikio.
(iii) Huathiri mifupa na meno.
**(iv)** Husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo **(ala 3 x1=3)**

(c)
- Madhara kwa njia ya uzazi huifanya iwe vigumu kuhimili.
- Ni rahisi kwao kuzaa njiti.
- Huzaa watoto wepesi
- Huweza kusababisha kifo cha mtoto aliye tumboni.
- Mtoto huweza kuzaliwa akiwa na kasoro.
- Mimba huweza kutunguka. **(alama 4 x 1=4)**

(d) Ndio: Kwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kwa sababu ya kutumia tumbaku/kwa siku watu 10,800 hufa. **(alama 1 x 2=2)**

(e)
- Ngozi ya mvutaji hukauka/fanya mtu kuonekana mzee.
- Vidole hugandwa na kutu ya sigara.
- Kucha za vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano/hudhurungi.
- Nywele hukosa nguvu
- Nywele hung'oka mapema. **(Zozote 3 x 1=3)**

(f) Kwamiliwa/kataliwa. **(1 x 1=1)**

**UFUPISHO** **(ALAMA 15)**

**2** a. i) Runinga ina manufaa yake

ii) Ni nyenzo mwafaka ya kufundishia

iii) Vipindi vinavyopeperushwa huwa na mafunzo kwa kila mtu

iv) Huleta vipindi ambayo huwafahamisha watu mambo ambayo yanaendelea katika mazingira yao

iv) Ikitumika pamoja na michezo ya video husaidia katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha/kujielimisha

v) Michoro ya video huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuwafanya watu kuwa makini wanapofanya kazi

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

vi) Ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha

vii) Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro

viii) Hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu

ix) Hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jami

**( zozote 8x1=7, ut=1)**

b. i) Baadhi ya vipindi hujumuisha ujumbe usio na maadili
ii) Vijana mengi wamekopa na kuyaiga wanayoyaona katika runinga
iii) Matumizi yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia/ Huleta utengano wa kifamilia.

iv) Baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya
v) Ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi

**(Zozote 5x1=5, ut=1)**

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

a) Eleza maana ya kipashio kidogo cha lugha. (alama 1)

**Sauti ni kipashio kidogo cha lugha kinachoweza kutamkika.** **(alama 1/0)**

b) Andika maneno yenye sifa zifuatazo: (alama 2)

i) kikwaruzo ghuna cha ufizi, vokali ya chini-wastani, kizuiwa ghuna cha midomo, kiyeyusho cha midomo, irabu ya chini-kati

**zabwa** **(alama 1/0)**

ii) Kipua ghuna cha ufizi, kipasuo cha ufizi, irabu ya mbele-juu, nazali ghuna ya midomo, irabu ya nyuma-juu.

**ndimu** **(alama 1/0)**

c) Ainisha uamilifu wa kisarufi wa mofimu kwenye neno hili. (alama 3)

**Lilimjisha**

**li-mofimu ya ngeli**

**li-mofimu ya wakati**

**m-mofimu ya mtendwa**

**j-mzizi**

**ish-mofimu ya kauli ya kutendesha**

**a-mofimu ya tamati/kiishio** **(alama $^1/_2 \times 6=3$)**

d) Tunga sentensi **moja** kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi **tu.** (alama 2)

**-Kuonyesha nafsi ya kwanza wingi k.m Tulisoma**

**-Kuleta dhana ya kudhibitisha k.m Alinipa kalamu moja tu**

**-Kama kitenzi kishirikishi kipungufu k.m Sisi tu wazima**

**-Kama yambwa k.m Alitubariki**

**Mfano: Tulikuwa tu wazima kabla ya ugonjwa wa Korona.**

**nafsi t**

**Tanbihi: Mtahiniwa atunge sentensi moja** **(alama $2\times1=2$)**

e) Unda kitenzi kutokana na nomino toba kisha ukitungie sentensi. (alama 2)

**Toba-Tubu**

**Waumini wote walitubu dhambi zao.** **(alama $2\times1=2$)**

f) Yakinisha kwa kutumia kiambishi cha masharti ya uwezekano kwa wingi. (alama 2)

Usiposoma kwa bidii hutofaidika.

**Mngesoma kwa bidii mngefaidika.** **(alama 2/0)**

g) Tumia nomino ya ngeli ya mahali dhahiri pamoja na kivumishi kirejeshi cha kati kwa sentensi. (alama 2)

**Pahali panapopendeza panatufaa**

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**Kirejeshi cha kati kijitokeze kwa kitenzi**

**Tathmini majibu ya watahiniwa** **(alama 2/0)**

h) Andika kinyume cha sentensi hii. (alama 2)

Mjomba alimtwika mwanawe mzigo akabana mlango.

**Mjomba <u>alimtua</u> mwanawe mzigo <u>akabanua</u> mlango.** **(alama 2×1=2)**

i) Bainisha kijalizo katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Tajiri huyo shupavu ana magari makubwa mno.

**Tajiri huyo shupavu ana <u>magari makubwa mno.</u>**

**Kijalizo** **(alama 1/0)**

**Kijalizo husaidia kukamilisha maana ya sentensi na huja baada ya vitenzi vishirikishi**

j) Tunga sentensi kwa kutumia chagizo cha ulinganisho. (alama 2)

**Msichana mrembo alitembea <u>kitausi.</u>**

**Chagizo cha ulinganisho ni sawa na kielezi cha ki ya mfanano**

**Tathmini majibu ya watahiniwa** **(alama 2/0)**

k) Andika upya sentensi kwa wakati uliopita hali endelevu, kauli tendesheka. (alama 2)

Wenyeji wamewapokea wageni kwa taadhima.

**Wageni walikuwa wakipokezeka kwa taadhima na wenyeji.**

**au**

**Wageni walikuwa wanapokezeka kwa taadhima na wenyeji.** **(alama 2/0)**

l) Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili ya neno **tema**. (alama 2)

**-Tema ni kutoa kitu kinywani mfano chakula, mate**

**- Tema ni hali ya kukata kitu kama vile mti, mkono kwa mfano;**

**Alitema mate alipokuwa akitema mti kwa shoka.**

**Maana iwe dhahiri na iwe kwa sentensi moja.** **(alama 2×1=2)**

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

m) Ainisha aina ifuatayo ya sentensi kiutendakazi. (alama 1)

Safari imekuwa ikitusumbua sana.

**Sentensi ya taarifa/kauli** **(alama 1/0)**

n) Onyesha kiima na utambue muundo wake katika utungo huu. (alama 2)

Pesa zote zilihifadhiwa na mwekahazina shujaa.

**Mwekahazina shujaa- N+V**

**Kiima**

**Kiima huonyesha mtendaji** **(alama 2×1=2)**

o) Tumia kishazi tegemezi kwenye sentensi kuonyesha vigezo vifuatavyo. (alama 2)

**i) Wakati**

**Nyumba ilipojengwa, tuliishi ndani. (PO ya wakati itumike)** **(alama 1/0)**

**ii) Jinsi**

**Mwalimu alitutembelea tulivyotarajia jana.**

**Watoto wote walituzwa tulivyoona shereheni.** **(alama 1/0)**

**Tathmini majibu ya watahiniwa**

p) Changanua kwa kielelezo cha mistari. (alama 4)

Aliponijia kwa mkopo, nilikuwa nasali sebuleni

**S-KN+KT**

**KN-N/W+S̄**

**N/W- Ø**

**S̄-aliponijia kwa mkopo**

**KT-Ts+T+E**

**Ts-nilikuwa**

**T-nasali**

**E-sebuleni** **(alama $^{1}/_{2}\times 8=4$)**

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

q) Andika upya kwa kuanza na yambwa tendwa. (alama 2)

Mvua iliwanyea wanunuzi sokoni hivi majuzi.

**Wanunuzi walinyewa na mvua sokoni hivi majuzi. (alama 2/0)**

r) Tunga sentensi kwa hali ya kudunisha ukitumia kihusishi cha uhusiano. (alama 2)

**Kijikalamu cha kijitoto kimepotea.**

**Kijumba cha kijimama kitabomolewa.**

**Hali ya kudunisha ni sawia na hali ya udogo.**

**Kihusishi cha uhusiano ni sawa na kihusishi cha a-unganifu (alama 2/0)**

s) Eleza matumizi ya kiambishi po katika sentensi. (alama 2)

Achezapo anapofika sisi hushangilia.

**achezapo-hali ya mazoea**

**anapofika-wakati maalum (alama 2×1=2)**

t) Twasema oyee tunapofurahia jambo **simile/hario** tunapotahadharisha na **harambee** tunapotoa himizo. **(alama 2×1=2)**

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza maana ya usanifishaji wa lugha. (alama 2)

**Ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo ya lahaja za lugha na kuifanyia marekebisho ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi ili iweze kutumika katika shughuli rasmi. (alama 2/0)**

b) Taja lahaja zozote mbili za kati. (alama 2)

**Kimvita-Husemwa Mombasa kisiwani**

**Kijomvu-Husemwa maeneo ya jomvu, nje ya Kisiwa cha Mombasa**

**Kingare-Husemwa Mombasa (alama 2×1=2)**

c) Maafisa watatu wa polisi jana walikana mashtaka ya mshukiwa wa mauaji ya watoto 13 kutoroka kutoka kituo cha polisi.

i) Tambua sajili inayorejelewa. (alama 1)

**Sajili ya matangazo/matangazo ya redio/matangazo ya runinga/ Sajili ya magazetini**

**(alama 1/0)**

ii) Eleza sifa **tano** za sajili hii. (alama 5)

**-Mada/anwani huwa fupi na yenye mvuto**

**-Matumizi ya tarakimu mfano 13**

**-Matumizi ya lugha ya kuvutia**

**-Ujumbe huandikwa au husomwa kwa aya fupi fupi ili kuokoa muda.**

**-Sentensi aghalabu huwa ndefu kwa lengo la kufafanua.**

**-Mara nyingi hutumia wakati uliopita.**

**-Matumizi ya lugha sanifu**

**-Matumizi ya lugha nyepesi/rahisi ili kueleweka**

**(Hoja za kwanza 5 alama 5×1=5, Asipofafanua atuzwe $^1/_2$)**

visit www.freekcsepastpapers.com to download free resources